BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi – Tarehe 23 Mei, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa Mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

74. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Baraza la Mji la Mkoani limekuwa likikusanya mapato kupitia vianzio vyake vinavyotokana na mali asili mbali mbali katika shehia ya Mwambe, Mchakwe na Jombwe kama vile mawe,

kifusi, kokoto na vingine vingi.

(a) Je, kuna mradi wowote uliofanyika katika shehia hizi kwa muda wa miaka 2 ya hivi karibuni.

(b) Je, tutegemee lini kutakuwa na mradi wa maendeleo kwa wananchi wa shehia hizo.

## Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

93. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ripoti za kila mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zinaonyesha mapungufu makubwa yanayozidi kukua mwaka hadi mwaka yanayosababishwa na ukosefu au uhaba wa viwango bora vya ukaguzi na uhasibu nchini.

(a) Je, kwa kiasi gani kada ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu iko imara Zanzibar.

(b) Je, ni chombo gani kwa Zanzibar kinahusika katika kuweka viwango vya kitaaluma, viwango vya ndani vya taarifa za fedha (Financial Reporting Standards) na viwango vya kimataifa vya kanuni za uhasibu.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuanzishwa kwa chombo bora na maalumu cha kuweka viwango vya kitaaluma kwa nia ya kujenga mfumo bora kiuhasibu, kiukaguzi na uwekaji wa taarifa za fedha utakaoendana na mfumo wa kodi, fedha na uwekezaji wa Kitaifa na Kimataifa.

95. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na mkanganyiko wa mara kwa mara kuhusiana na mfumo wa ukusanyaji wa kodi na mapato mengine ya Serikali na kurejesha kiasi cha fedha kinachotakiwa kubaki kwa taasisi husika. Aidha, kumekuwa na ucheleweshwaji mkubwa au kutopelekwa kabisa kwa mapato yanayotakiwa kurejeshwa kwa taasisi husika.

(a) Je, kwa mwaka 2022/2023, Serikali imekuwa ikitumia mifumo ipi ya kukusanya kodi na mapato mengine ya Serikali.

(b) Je, ni kwa kutumia utaratibu na mfumo upi Serikali hurejesha kiasi stahiki cha fedha kutoka kwenye fedha iliyokusanywa na taasisi husika.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuwa na mfumo bora wa kielektroniki wa kifedha unaowezesha kufanyika kwa mgao wa mapato kwa taasisi husika bila ya kuingiliwa na michakato mengine.

<u>**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**</u>

105. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusiana na athari zinazoendelea zinazosababishwa na umeme usioaminika na usiotulia (Power Instability) ambapo kwa kiasi kikubwa huleta athari kwenye upatikanaji wa maji kwa kuunguza mara kwa mara mashine za kusukumia maji, kuungua kwa vyombo vya kielektroniki na umeme vinavyotumiwa majumbani na hata uunguaji wa transfoma. Kwa kuwa jambo hili limekuwa endelevu bila ya kupatiwa ufumbuzi.

(a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea umeme wa Unguja na Pemba kukosa utulivu (stability) hasa umeme wa mtumiaji wa mwisho.

(b) Je, Serikali imefikiria nini juu ya kulitatua suala hili kwa muda na kwa kudumu.

(c) Je, ni lini wananchi wategemee utatuzi wa suala hili sambamba na tathmini ya wastani wa uharibifu unaosababishwa na hali ya sasa ya kutotulia kwa umeme unaotumiwa na wananchi majumbani.

<u>**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**</u>

59. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kinyakuzi na Saninga ni mabonde ya umwagiliaji ambayo wananchi wa shehia za Chimba, Kinowe na Tumbe wanayategemea sana kwa shughuli zao za kilimo cha mpunga. Hata hivyo, kwa miaka mingi sana wananchi hawa hawapati mavuno kutokana na miundo mbinu yake kuharibika sana.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali inalifahamu tatizo hili.

(b) Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya kadhia hii.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

129. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Inaaminika kwamba kwa nchi kama Zanzibar ili isonge mbele kiviwanda, ni budi iwe na sera ya viwanda inayoendana na mabadiliko ya ulimwengu pamoja na kuweka mahusiano mazuri ya viwanda na mashirika ya Serikali. Aidha, Baraza la Taifa la Viwanda Zanzibar (Zanzibar Industrial Council) likiwepo, linaweza kuimarisha ushirikiano wa dola na jamii pamoja na kuweka kipaumbele katika kukuza sekta ya viwanda kwa mambo yanayohusiana moja kwa moja na maliasili za Zanzibar. Hata hivyo, kasi ya kuyaendea hayo imekuwa ndogo sana.

(a) Je, Serikali imewahi kufanya utafiti kwa karibuni kutambua viwanda ambavyo vitaweza kuanzishwa na kuendeshwa bila ya kutegemea rasilimali (raw materials) kutoka nje ya Zanzibar.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuvifufua viwanda vidogo vidogo ambavyo vilikuwepo japo kwa namna nyengine ya usimamizi.

(c) Je, Serikali haioni ulazima wa kuunganisha viwanda na taasisi za utafiti na elimu ili kupatikana elimu ya vitendo kwa wahitimu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

14. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Takriban muda mrefu sasa umepita tangu Serikali ilivyotoa ahadi ya kuijenga barabara ya Wawi Mesi, Vikunguni hadi Uwandani.

(a) Je, ujenzi huo unatarajiwa kugharimu kiasi gani cha fedha hadi kukamilika kwake

(b) Je, ujenzi huo unatarajiwa kuanza lini.

**Wizara ya Afya:**

110. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Vituo vya Afya vya Pandani, Maziwani, Kiungoni na Mzambarauni katika jimbo la Pandani, vinakabiliwa na changamoto mbali mbali zinazozorotesha huduma za afya tofauti na huduma kama hizo wanazopata wananchi wenzao katika vijiji vingine.

(a) Je, ni lini ukarabati au ujenzi mpya wa vituo vya afya vya Pandani, Maziwani, Kiungoni na Mzambarauni utaanza ili huduma zao ziendane na ongezeko la watu katika maeneo hayo sambamba na kuondokana na uchakavu wa vituo hivyo usioendana na matumizi ya binaadamu.

(b) Je, ni lini kabati (shelf) lililokosekana katika kituo cha afya cha Mzambarauni litapatikana ili kituo hicho kiweze kuanza kazi.

(c) Kwa vile mfanyakazi mmoja aliyepangiwa kazi kituo cha afya Maziwani alikataa kuripoti kazini na kusababisha kituo hicho kisianze kazi na kwa vile wapo wahitimu wenyeji wa jimbo la Pandani wanaoipenda Pandani, Je Serikali imechukua hatua gani kwa mtumishi huyo aliyekimbia na ni upi utaratibu wa kuajiri mfanyakazi mwengine mwenyeji wa jimbo la Pandani.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

6. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Imekuwa ni jambo la kawaida kwa vituo vyetu vya ZBC upande wa Televisheni kurusha vipindi ambavyo vinakosa mvuto kutokana na kosa la kuruka kwa vipindi hivyo pamoja na kuvirejea sana kama kwamba Zanzibar haiwezi kupata vipindi bora zaidi vitakavyohamasisha wananchi kuviangalia na kuvipa mgongo vipindi vya vituo vyengine vya nje ya Zanzibar.

(a) Kwa nini hadi leo Serikali imekosa wahisani wa kukifadhili kituo hicho.

(b) Je, imefikia wapi mipango ya kuwawezesha kielimu wafanyakazi wazalendo ambao watatayarisha vipindi hivi kiueledi.

(c) Kwa nini hadi sasa hatuna vipindi endelevu kama michezo inayotafsiriwa kwa lugha yetu ambayo inachezwa nchi nyengine ukiachia mbali ile ya wa china.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

37. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa tatizo la utoro huchangiwa na sababu nyingi zikiwemo upungufu wa walimu maskulini.

(a) Je, Wizara yako ina upungufu wa walimu wangapi kwa Unguja na Pemba.

(b) Je, ni walimu wangapi wamebahatika kuajiriwa katika Bajeti ya 2022/2023 kwa upande wa Pemba na Unguja.

(c) Je, kwa kiasi gani ajira hizo zimezingatiwa uwiano (ratio) kulinganisha na uhaba mkubwa wa walimu wa baadhi ya maskuli.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

133. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Biashara na shughuli za utalii zinahitaji kutangazwa na kuuzwa kimkakati. Hata hivyo, umuhimu wa suala hili haujaoneshwa kwa vitendo kwa sababu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli hizo haujaonekana katika mahitaji ya dharura na muhimu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti na unaotekelezeka wa kuutangaza utalii wa Zanzibar.

(b) Je, Serikali imewahi kufikiria kwa uzito wake suala la kuzindua ‘slogan’ ya maonesho ya kimataifa ya utalii.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuandaa mfumo maalum wa usafiri wa bure kwa watalii watakaotembelea maeneo ya mji mkongwe kama njia ya kuwaonyesha ukarimu na kuwapa urahisi wa kuuona urithi muhimu wa nchi yetu na dunia kwa ujumla.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
23 Mei, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA